HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

MAFINGA

KUMB. NA. MTC/CHSS/JI/2021/F1/07 11/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI……

S.L.P. ……

……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO HALAMSHAURI YA MJI MAFINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na KIDATO CHA KWANZA katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Changarawe ipo umbali wa kilometa 4 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Mafinga Mjini – bara bara iendayo MAKAMBAKO – NJOMBE – MBEYA, iliyoko Mafinga katika Halmashauri ya Mji Mafinga.

Usafiri wa Teksi kutoka Mafinga Mjini mpaka shuleni unapatikana katika kituo cha MABASI – Mafinga (SEMA UPELEKWE CHANGARAWE SEKONDARI).

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11.01.2021** unatakiwa kuripoti shuleni Tarehe **06.01.2021.**

2.0 MAMBO YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

WAVULANA

a) Sare ya shule hii kwa wavulana ni:-
   - Suruali American Khaki mbili (02) zilizoshonwa kwa Heshima.
     - Mshono wa mifuko aina ya jeans hauruhusiwi
     - Mshono wa suruali mlegezo hauruhusiwi
     - Mshono wa suruali unaotakiwa uwe na upana nchi 21 na kuendelea
     - Suruali isiwe modo (ya kubana) haitapokelewa. (KITAMBAA KIMEAMBATANISHWA).
     - Mashati meupe mawili (02) mikono mirefu yasiyoangaza
     - Viatu vyuesi vya kufunga na kamba
     - Soksi nyeusi bila maua au marembo mengine (JOZI MBILI)
     - TAI MOJA rangi ya kahawia (Dark Brown).(isiyo na maua au urembo wowote)
     - SWETA – Rangi ya kijani yenye V-shape (MOJA)
     - Mkanda wa suruali mmoja (01) mweusi wa kawaida (usio na urembo, picha, nembo au alama zozote zile)

b) Sare ya michezo kwa shule ni BUKTA RANGI YA BLUU MOJA (01), FLANA YA NJANO MOJA(01) NA RABA PEA MOJA. (Kwa wavulana na wasichana)

c) TRUCK SUIT NYEUSI (YENYE MISTARI MIEUPE)

WASICHANA

a) Sare ya shule hii kwa wasichana ni
   - Sketi (02) rangi ya kahawia (DARK BROWN) ILIYOSHONWA KWA Heshima . iwe ndefu, inayofika fundo la mguu – iwe na rinda za kawaida KUMI NA SITA (RINDA BOKSI KWENYE SKETI HAZIRUHUSIWI).
   - Blauzi mbili (02) nyeupe mikono mirefu isiyoangaza
   - Viatu vyeusi vya kufunga na kamba (Boots, viatu vya kuchomeka haviruhusiwi)
   - Soksi jozi mbili(02) rangi nyeupe bila maua
   - Sweta moja rangi ya kijani yenye V- Shape
   - Tai moja rangi ya kahawia (Dark –Brown) (Isiyo na maua au urembo wowote)
   - **TRUCK SUIT NYEUSI (YENYE MISTARI MIEUPE)**

b) HIJABU

- Wanafunzi wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe na kitambaa cha ndani cheupe na si rangi nyingine yoyote ile.
  - ❖ **CHETI CHA KUZALIWA**
  - Kila mwanafunzi aje na NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA

2.2. **VIFAA VYA MASOMO**

- Daftari kubwa kumi
- Peni na kalamu
- Mkebe wa Hesabu

2.3 - Chakula cha wanafunzi wa kutwa kamati ya chakula ya wazazi itaelekeza
- Pia utamhudimia mwanao nauli ya kwenda na kurudi nyumbani na matibabu endapo ataugua.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, na Mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.

3.**2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Wizi
b) Uasherati, ushoga na usagaji
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Medica Examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi, kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

NB: FOMU ZIMEAMBATANISHWA

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

LULU H. NGATUMBURA

MKUU WA SHULE

FOMU NA. 02. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANFUNZI /MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

.....

.....

.....

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126.

MAFINGA

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA-MKOA WA IRINGA

Mimi mwanafunzi……. Kidato cha …….. Mwaka……

1. Nilizaliwa mnamo mwaka (Taja tarehe, mwezi na mwaka)…….. kijiji/Mjini……..
   Nimesoma shule ya msingi ya …….. Wilaya ya …….. Mkoa wa ……..
   - Nilikuwa kiongozi wa ……
   - Sikuwa kiongozi……
   - Michezo niipendayo ni ……
   - Ninakipaji cha…….
   - Mengineyo Niwezayo…….

2. Naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, dharau kwa walimu, dharau kwa viongozi wa ngazi zote au wowote wale.
   Nakuwa na nidhamu ya kujituma, kusoma kwa bidii na kwa mfano bora kwa wanafunzi wengine. Tofauti na haya niondolewe shulenimara moja.

   Jina la mwanafunzi…… sahihi…… kidato……... tarehe ……

FOMU NA. 3. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA , KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE HALALI YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

……

……..

……..

…….

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

MAFINGA

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA MWANANGU NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA-MKOA WA IRINGA

MWANAFUNZI ……

KIDATO CHA …….. MWAKA……

1. Mimi …….
   Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Nakiri kuwa nimeelewa maelekezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu aendelee na masomo na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake. Kama ilivyoagizwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidhi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapa shuleni.
5. JINA LA MZAZI / MLEZI …… SAHIHI……..
6. ANWANI YA MZAZI/MLEZI…….
7. NAMBA YA SIMU …… TAREHE ……

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

FOMU NA. 01. (FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI)

SEHEMU A

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

MAFINGA

KUMB.NA.MTC/CHSS/JI/2021/F1/07 11/12/2020

MGANGA MKUU,

HOSPITALI YA SERIKALI YA

……..

S.L.P……..

MAFINGA

YAH: FOMU YA KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI

Somo la hapo juu lahusika.

Tafadhari tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu wa kidato cha KWANZA mwaka 2019; kwa gharama za mzazi/mlezi wake.

Ni muhimu apimwe ili kujua afya yake kabla ya kuripoti hapa shuleni na kendelea na masomo.

Natanguliza shukrani

……

LULU H. NGATUMBURA

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI

SEHEMU B

YAH: MWANAFUNZI……

<u>WA KIDATO CHA KWANZA, MWAKA 2021</u>

Matokeo ya vipimo vya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu ni:-

……

……..

……

……..

Nathibitisha kuwa ……..

……

……

JINA LA MGANGA……

CHEO……

SAHIHI…… MUHURI…… TAREHE……